**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MNYUZI.

**Juni, …………….**

**KOROGWE, TANGA - TANZANIA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE,**
**SHULE YA SEKONDARI MNYUZI**


**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule; 0739998880; 0768866266, 0658600066**

**Makamu Mkuu wa Shule. 0752892055;**

**Matron; 0687363090 [Kibumu]**

**0789524495.[Moshi]**

**SHULE YA SEKONDARI MNYUZI,**
**S.L.P 314 KOROGWE-TANGA,**
**EMAIL; mnyuzisec06@gmail.com,**


**Tarehe ………….**

**Kumb. Na. MNYZ/JOI/2025/02.**
Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi ………………………………………………………………………

S.L.P………………………………………………………………………………

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MNYUZI HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE. MKOA TANGA, MWAKA ……………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya sekondari ya MNYUZI ipo umbali wa kilometa 22 kutoka kituo cha mabasi cha Wilaya ya Korogwe. Usafiri unapatikana katika kituo cha mabasi cha mji wa korogwe kuanzia asubuhi hadi saa 12:00 jioni nauli ni shilingi **5,000 Bajaji**. Shuka Mnyuzi. Chukua Bodaboda/Pikipiki Nauli **1,000/=** ikupeleke shule ya sekondari ya ***MNYUZI (kwa waliopanda magari yanayotoka Arusha au Dar es salaam nakushuka stendi Korogwe), Kwa wanaotoka Tanga shuka KITUO cha magari MAGUZONI kisha chukua pikipiki nauli 3000 Hadi shuleni.***
***NB. TUNASHAURI KWA WANAFUNZI WOTE WANAOTOKA NJIA YA ARUSHA AU DAR ES SALAAM, AU MOROGORO WOTE WAPANDE MAGARI YANAYOENDA TANGA MJINI KISHA WASHUKIE KITUO KINACHOITWA MAGUZONI, UKISHUIKA KOROGWE MJINI UTAONGEZA GHARAMA.WASILIANA NA UONGOZI SIKU UNAPOKUJA SHULE ILI UELEKEZWE VYEMA***.

**KUMBUKA UKICHELEWA HATA SIKU MOJA MASOMO YATAENDELEA HAYATAKUSUBIRI, FANYA MAANDALIZI MAPEMA RIPOTI KWA WAKATI.**
**NB. MZAZI/MLEZI Mwandalie mapema mwanao mahitaji yake** na aripoti mapema maana masomo yataanza wiki ya kwanza.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni **SKETI** kwa Wasichana rangi ya **OLIVE GREEN (HEX708238, RG 11213056).** Maelezo ya mshono na kuepuka mkanganyiko wa rangi ya sketi na mashono **Endapo utakosa** zinapatikana karibu shuleni **wasiliana na Matron**. **Suruali Kwa Wasichana Hairuhusiwi Kabisa**. Mshono wa sketi na gauni ni rinda box 4**,** Sketi Itakuwa Ndefu Iguse Kiwiko/Kifundo/kisigino Cha Mguu Kwa Wanafunzi Wote, Usishone Kwa Mazoea au unavyojua au ulivyoona, **Fuata Maelekezo** Tuliyotoa (**sketi au gauni fupi isiyozingatia maelekezo haitakubalika na hutaruhusiwa kutumia shuleni**), kuepuka hasara ya kukosea rangi au mashono unashauriwa kuja kushona karibu na shule ambapo shule itasimamia.

ii. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu aje nayo

iii. Hijabu rangi nyeupe (tetron) Kwa mwanafunzi Mwisilamu. Hijabu iwe nyeupe isiwe na urembo wa aina yoyote au kufungwa na urembo wowote Hijabu Iwe Ndefu Ifunike Mikono Akishusha Chini**.** Unaweza kushona hijabu AU **endapo utakosa** kununua dukani .

iv. Sare ya Michezo ni **(a).** T-sheti nyekundu isiyo na picha, mchoro wala maandishi **(b).** Bukta rangi ya Blue. **(c).** Sketi ya rangi ya Orange ya kuzunguka kwenye bukta Urefu wake **ivuke goti kwa urefu wa inch 6** (usivae nguo hii nje na shughuli ya michezo pekee na hasa siku na saa ya michezo tu ndipo uvae) **(d)** Raba nyeupe au nyeusi, raba ziwe za kufunga na kamba

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

vii. Sweta rangi ya Zambarau mikono mirefu, iwe na **V** shingoni

viii. **viii.** Nguo za kushindia **(a)** Track suit rangi ya blue (**Dark Blue**) itatumika pia kwa kushindia, kusomea usiku pamoja na gauni .(IWE NZITO) (**b**) Gauni mbili mikono mifupi **rangi ya damu ya mzee** liwe refu ukisimama **liguse** kisigino cha mguu, isiyoonesha uwazi mzunguko wa shingo, na lisibane mwili) sketi ndiyo nguo utakayovaa siku unaporipoti shuleni au truck suit NGUO ZOZOTE ZA NYUMBANI USIJENAZO SHULENI hutaruhusiwa kuvaa shuleni.

ix. Tisheti (T-shirt) ya shule Yenye nembo ya shule zinapatikana shuleni.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari makubwa 15 Quire 3, kalamu za kutosha ma mathematical set moja. **NB. Nunua Madaftari**
ii. **Kabla Ya Kitu Kingine Chochote.**
iii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi yako.

**<u>Njoo na vitabu vya combinationyako muhimu sana.</u>**

**HISTORY –**

I. *Advanced History for secondary schools student's book Form Five (TIE).*

II. *Advanced History for secondary schools student's book Form Six (TIE).* III.Literature books - TIE

➢ Major events in the world History by Gervas

➢ Kato, A (2011) Mastering Advanced Learners History for Form 5&6

➢ Oxford (2011) Advanced Learners History Form 5 & 6 Zombwe

**GEOGRAPHY -**

1. *Physical geography for Advanced secondary schools student's book Form Five and Six (TIE).*
2. *Human geography for Advanced secondary schools student's book Form Five and Six (TIE).*
3. *Practical geography for Advanced secondary schools student's book Form Five and Six (TIE)*

(a) Contemporary issue in Geography by Msabila

(b) (b) Integrated approach Geography

© Essential of practical Geography Advanced level (Form 5 & 6 )

➢ Zist, K (2015) ,Geography Paper Two, Human and Economic Geography

➢ Zist, K (2016), Physical Geography Paper One

**KISWAHILI**

- *Kiswahili shule za secondari kitabu cha mwanafunzi kidato cha Tano na Sita(Taasisi ya Elimu Tanzania).*

**Riwaya:** Vuta ni kuvute, Usiku utakapokwisha,Mfadhili na Barua ndefu kama hii.

**Ushairi:** Kimbunga, Na Chungu Tamu. **Tamthilia:** Nguzo mama, Kwenye ukingo wa thim, Morani

➢ Oxford University Press (2012) Kiswahili Kidato cha Tano na Sita

➢ Nyangwine Nadharia ya Lugha Kiswahili 1 Kidato cha 5 na 6

➢ J .A. Masebo (2006) Nadharia ya Fasihi Kiswahili 2 Kidato cha 5 na Sita

➢ Tahakiki vitabu teule vya Fasihi kidato cha Tano na Sita J. A Masebo&Nyambari Nyangwine 2008

➢ **KAMUSI YA**– Kiswahili ya TUKI

**GENERAL STUDIES -**

■ *General studies for Advanced secondary schools student's book Form Five and Six (TIE).*

➢ Mwajabu, M (2016) Comprehensive Book for Advanced Level Secondary School

➢ Nyambari, N & Bukagile, R (2010),Contemporary Approach for Advanced Level General Studies Form 5&6

**ENGLISH:**

- *English for Advanced secondary schools student's book Form five (TIE)*
- *English for Advanced secondary schools student's book Form Six (TIE).* ➢ English Paper One. Ashel, N (2010): Advanced Level English a practical Approach

➢ Paper Two. Ashel N (2011) Advanced Level Literature An Essential Guide

➢ Nyambari Nyangwine (2008): Advanced Level Literature

✧ **English Advanced Dictionary.**

***NB.***

❖ ***VITABU HIVYO NI MALI YA MWANAFUNZI, WALAU KITABU KIMOJA KWA SOMO AU ZAIDI***

❖ ***KWA MZAZI ANAYEPENDA MWANAYE AFAULU KWA VIWANGO VYA JUU MNUNULIE MWANAO VITABU MUHIMU, VITABU BORA NI VILE VILIVYOANDALIWA NA TAASISI YA ELIMU TANZANIA ( TIE).***

❖ **REVIEWS** – HISTORY 1 & 2, GEOGRAPHY 1& 2, KISWAHILI 1&2, GENERAL STUDIES

iv. Njoo na Godoro ich 4 ya futi 2.5 / 6.

v. Mashuka Jozi 2 rangi pink, blanket 1, foronya ya mto1 rangi pink, chandarua 1 rangi nyeupe*;*

vi. Nguo za ndani za kutosha;

vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe). ***Vyombo vya chakula vya Plastiki havitakiwi shuleni***) vyombo vinavyohitajika ni vya **bati,** pia uje na dumu la lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa na chupa maalum ye kubebea maji ya kunywa mchana uwapo shuleni,

viii. Ndoo 2 ndogo za shule (lita Kumi) zenye mifuniko na ndoo moja 1 au zaidi ya mwanafunzi kadiri ya matumizi yake;

ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, Hard Bloom 1, Soft Bloom 1, Squeezer 1.

x. **Tochi ndogo** dharura za usiku (Tochi ya kuchaji na jua ni bora kuepuka kununua betri kila wakati)

xi. Taulo, malapa, mswaki, kanga/vitenge vitatu, nguo ya kulalia ambayo huruhusiwi kutoka nayo nje ya bweni na mahitaji mengine muhimu ya mtoto wa kike.

xii. Uje na mafaili 3 kwa ajili ya matumizi ya shule na mwanafunzi.

xiii. Uje na kitambulisho cha bima ya afya **NHIF** au **CHF** iliyokatwa ndani ya **mkoa wa Tanga**. Kama huna Bima uje na TSH.50,400/= kwa ajili ya Kukatiwa Bima CHF ndani ya Mkoa wa Tanga.

### 2.3 Michango mbalimbali

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo za Michango jumla yake kwa mwaka ni 80,000/= ZITALIPWA AKAUNTI YA SHULE, **NMB 41501200063** JINA **SHULE YA SEKONDARI MNYUZI**, LIPA KWA NJIA YA BENKI, WAKALA WA BENKI. MAJINA YA MLIPAJI YAWE MAJINA MWANAFUNZI KWENYE RISITI YA MWANAFUNZI NA JINA LA MWEKAJI SIYO LA NDUGU AU MZAZI.

**N.B. KAMWE USITUME FEDHA HIZI AU KULIPA MKONONI KWA MWALIMU YEYOTE**. Mwanafunzi aje na Bps (karatasi ya malipo Benki nakala Halisi (original) toa copy / nakala ya kila malipo ubaki nayo nyumbani kwa kumbukumbu zako mwenyewe.

NB. Kama unalipiwa na mfadhili yeyote ajitahidi kukulipia kabla ya kuripoti shuleni.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki au kukaa navyo **vifaa vyenye ncha kali na dawa yeyote bila taarifa au idhini kutoka kwa uongozi wa shule;** na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Hakutakuwa na ruhusa ya kuzurura (outing) nje ya shule katika siku za masomo (uwapo shuleni), ILA kunaweza kukawa na **ZIARA Rasm**i za wanafunzi zitakazogharimiwa na wazazi kwa lengo la mafunzo nje ya shule zenye ruhusa rasmi za mamlaka zinazohusika.
xiii. Siku za ibada utafanya ibada shuleni na nje ya shule kwa kibali maalum chini usimamizi wa walimu walezi, muda wa ibada ukiisha wahi shule bila kuzurura mtaani au kwenda katika nyumba za watu wengine ikiwemo walimu ni kosa. Wanafunzi wataambatana na walimu walezi wa imani zao kama hakuna mwalimu mwanafunzi atafanya ibada yake shuleni kuzingatia usalama wa wanafunzi bila usimamizi.

**MUHIMU:**

❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu,** redio, na pasi ya umeme, au kifaa chochote kinachotumia umeme **shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;** , Ukikutwa na simu ya mkononi, “line/chip” Ya simu au “smart watch” yenye uwezo wa simu mahali popote ndani ya eneo la shule au nje ya shule kwa muda/siku za masomo kabidhi kwa liyekukamata upesi, utafukuzwa au kusimamishwa shule wakati huohuo, simu na line itakayokamatwa shuleni itahesabika kama kusudio la kuleta madhara katika rasilimali zingine za shule, utalipa *faini kadiri ya itakavyoamuliwa* si chini ya150,000/= kama simu italeta madhara utalazimika kulipa gharama ya hasara uliyosababisha pamoja na faini.

- Kwa mawasiliano na wazazi mwanafunzi atumie simu ya **Mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule (utawala), Mwalimu wa fedha(fedha za shule), Mwalimu wa nyumba (matron (mahitaji binafsi)**, mwafunzi haruhusiwi kutumia simu ya mtu mwingine nje na waliotajwa, ikitokea mwanafunzi ametumia simu ya mtu asiye mwalimu nje au ndani ya shule atafukuzwa shule au kusimamishwa shule au adhabu kali.
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- Mwanafunzi atakayetoroka Bwenini au shuleni, au kuagiza vitu au kifaa, kitu chochote nje ya shule bila Ruhusa au kibali cha walimu atafukuzwa shule mara moja kwa kuhatarisha usalama wake na usalama wa shule.

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele hakuruhusiwi shuleni. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA MNYUZI SEKONDARI**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule** **<u>WILLIAMN.SULLE</u>**

HEADMASTER
MNYUZI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX
KOROGWE

**<u>Muhuriwamkuuwashule</u>**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule; 0768866266**
- **Makamu Mkuu wa Shule; 0752892055**
- **Mwandamizi Taaluma; 0743271978**
- **Mwandamizi Malezi; 0766506895**

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (V).**
**SHULE YA SEKONDARI MNYUZI**

**S.L.P 314,**
**KOROGWE.**
**TAREHE ……………**

**(C). FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIYOPEWA.**

**SEHEMU A**; **Taarifa za mwanafunzi.**

1.Jina kamili (mwanafunzi)…………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa (mwanafunzi) ……………………………………………

3. Wilaya alipozaliwa (mwanafunzi) ………………………………… kata ……………………………..
kijiji…………….……………

4. Kukubali nafasi**. (Ijazwe na mwanafunzi)**

Mimi (Jina la mwanafunzi) ………………………………………………………………nimesoma na kuelewa maagizo yote ya shule ya sekondari ya Mnyuzi na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule. Nitakapokuwa shuleni Mnyuzi nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata Elimu ya kujitegemea.

**Sahihi ya mwanafunzi …………………………………. Tarehe …………………………………….**

**SEHEMU B; Taarifa** za **mzazi/mlezi(Ijazwe na mzazi /mlezi**).

1. Jina kamili la mzazi/mlezi……………………………….…………………
2. Mimi ni mzazi/mlezi? ……………………….…………………………….
3. Kazi yako ……………………………………………………………………
4. Anwani ya mzazi/mlezi. …………………………………………………
5. Namba tatu za simu ya mzazi/mlezi wa mwanafunzi

(a)…………………………….…………(b)……………………………(c)………………….……………
……

**UTHIBITISHO**

**M**imi.mzazi/mlezi wa………………………………………………………………… Nimehakikisha kwamba maagizo yote yameeleweka na mtoto wangu amejaza kikamilifu **sehemu A hapo juu.**

**Sahihi ya mzazi/mlezi……………… Tarehe…………………………………………………**

**Taja Majina na simu za ndugu wengine au mzazi anayeweza kumtembelea mwanafunzi shuleni na inapotokea tatizo.**

**1.Jina ……………………………………………………..simu………………………., …………..**
**2.Jina ………………………………………………………simu …………………….., …………**
**3.Jina ………………………………………..simu ………………………..,……………**

**NB.** **<u>FOMU HII IWE IMEJAZWA NYUMBANI NA MZAZI PAMOJA NA MWANAO, UTAIKABIDHI FOMU HII SIKU YA KWANZA UNAPOKUJA KUMKABIDHI (kuripoti)MWANAOSHULENIIKIWAIMEJAZWATAARIFAZOTEMUHIMU.</u>**

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE (V).**
**SHULE YA SEKONDARI MNYUZI**

**(B). REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

**MNYUZI SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.BOX 314,**
**KOROGWE.**
**DATE…………………………..**

**MEDICAL OFFICER,**

………………………………. GOVERNMENT HOSPITAL. (**Jina la Hospitali ya serikali**).

**NAME OF STUDENT: ………………………………………………………………………**

Please examine the above named student to ascertain his/her fitness for further studies.

………………………… **HEAD OF SCHOOL.**

**MEDICAL CERTIFICATE:**

[To be completed by the medical officer].
I have examined the above named students with regard to: Skin …………………………… Eyes ,……………………… Ear………………Chest……….………Eyes ……………………………
Spleen ………………… Abdomen ……………………
Urine ………………………………………Stool …………………………
Hemoglobin ……………………… Sickle ……………………… cell ………………………………
others……………………
**UPT…………………**

**Hepatitis B. …………..**

**And I considered.**
**1.**He/She has good health, free from infection diseases, worms, bilharzia, and fit to go to school.
**2.** He/She can return to school/home having treatment ……………………………………………

Name……………………..……………………….. & signature………………. of medical officer
**Date:** ……………………………………………………………

**NB.** FOMU HII IWE IMEJAZWA NA **DAKTARI WA HOSPITALI YA MKOA, WIALAYA AU KITUO CHA AFYA CHA SERIKALI NA KUGONGWA MUHURI AMBATANISHA RISITI YA SERIKALI YA MALIPO YA VIPIMO TAJWA, UTALETA FOMU HII SHULENI SIKU YA KWANZA UNAPOKUJA KUMKABIDHI (kuripoti) MWANAOSHULENI.**